

Nafasi ya Ontolojia ya Kiafrika katika Jamii ya Wanyakyusa Nchini Tanzania

Gerephace Mwangosi
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
gerephacem@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza nafasi ya ontolojia ya Kiafrika kwa kurejelea jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya mahojiano na usaili katika wilaya ya Rungwe na halmashauri ya Busokelo. Nadharia ya Usosholojia ilitumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa. Matokeo ya makala hii yanaonesha umuhimu wa ontolojia ya Kiafrika katika kuijenga na kuiendeleza misingi imara ya kimaadili, kifalsafa na kiutamaduni ili kuyakabili maisha na mazingira yao. Pia, inatazamwa kama maktaba mahsusi ya ufafanuzi na urejelezi wa masuala ya kiasili na kiutamaduni yanayotumika kama kiungo thabiti cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi imara ya kimaisha na kimazingira. Makala hii inahitimisha kuwa falsafa ya Kiafrika imejikita katika masuala ya kiontolojia ya kila jamii kwa kuchunguza hali, kanuni za uhalisi, chimbuko, kanuni na hatima ya kuwapo kwa watu, vitu au maumbile.

Maneno Msingi: Ontolojia ya Kiafrika, Wanyakyusa, Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika.

Utangulizi

Kwa muda mrefu, kumekuwa na mawazo yanayokinzana kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa falsafa ya Kiafrika. Wataalamu wa Kimagharibi wanashikilia kuwa Waafrika hawana falsafa yao kwa kuwa hawakuwa na maandishi (Bodunrin, 1981). Msingi wa hoja hii unafungamana na madai kuwa Waafrika hawana uwezo wa kufikiri kutokana na kuwapo kwa mila zisizozingatia tafakuri za kirazini. Pia, wanaona kuwa kile kinachoitwa falsafa ni mila, uchawi, miviga, imani, miiko, itikadi na simulizi na si tafakuri razini zinazoweza kuitwa falsafa (Hontondji, 1983). Mtazamo huo uliasisiwa na Wakoloni ili kuhalalisha harakati zao za kuitawala Afrika katika nyanja zote bila ya kutazama hatua za kimaendeleo ilizokuwa imezifikia kabla ya ujio ya wageni hao.

MAKALA HALISI

HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 13 Julai 2021

Kurekebisha: 30 Sept. 2021

Kukubaliwa: 21 Oktoba 2021

Kuchapishwa: 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 62 – 73.

NUKUU: Mwangosi, G. (2021). Nafasi ya Ontolojia ya Kiafrika katika Jamii ya Wanyakyusa Nchini Tanzania. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, 7(2), 62 – 73.

Pia, wanadai kuwa falsafa ya Kiafrika imejiegemeza katika mapokeo ya watu wa Magharibi. Mtazamo huo ulipingwa na Oje-Ade (2004) anayeeleza kuwa falsafa ya Kiafrika ni ile inayohusu dhamira za Kiafrika na mbinu zinazoitofautisha na mataifa mengine. Jamii za Kiafrika, kama zilivyo jamii nyingine ulimwenguni kote, zina falsafa yao iliyoundwa na vipengele vya eskatolojia, epistemolojia na ontolojia ambavyo hubainika katika fani za fasihi. Pia, inachanganya vipengele vya udhanifu na uyakini na ina mikondo mbalimbali (Faustine, 2017). Falsafa ya Kiafrika ilianza kubadilika baada ya ujio wa wageni katika bara la Afrika. Ujio wao ulisababisha Waafrika kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha zao, majina yao, rangi, vyakula, tamaduni na mila zao. Falsafa ya Kimagharibi ilitoka hisia za ukengeushi katika mazungumzo, utamaduni, elimu, dini na mitindo ya maisha (Masolo, 1994). Mwingilano huo uliathiri utambulisho wa Mwafrika ulioingia katika nyavu za utatanishi.

Falsafa ya Kiafrika inahusu masuala mbalimbali yanayomhusu binadamu, kuwapo kwake na hatima ya maisha yake (Mages, 1997). Pia, inaweza kuwekwa katika mikondo kadha (Mulokozi, 2017). Kwanza, falsafa ya Kifasihi inayobebwa katika tungo na fani za fasihi simulizi na andishi. Pili, falsafa ya Kijadi inahusu tafakuri za jadi, hasa maisha, ulimwengu na kuwapo kwake. Hujitokeza pia katika mila, miviga na masimulizi. Tatu, falsafa ya Kitaaluma inayotokana na tafakuri za wasomi wa falsafa. Nne, falsafa ya Kihikimati inayotokana na tafakuri za wazee wenye busara na hekima. Tano, falsafa ya Kidiaspora inatokana na tafakuri za Waafrika walioko ugenini. Sita, falsafa ya Kisiasa inayohusu tafakuri ya maongozi na utawala zinazofanywa na baadhi ya watu, wakiwamo wanaharakati na wanasiasa. Mwisho, falsafa ya Kihemenitiki inayohusu uchunguzi wa miundo na mitindo ya lugha ili kupata falsafa.

Ontolojia ni taaluma ya falsafa inayoshughulikia asili ya kuwapo au kuishi kwa viumbe vinavyoonekana na visivyoonekana pamoja na maumbile ya ulimwengu (Mbiti, 1969). Mwafrika ndiye kiini cha ontolojia ya Kiafrika. Ontolojia inarejelea kuwapo kwa mtazamo na imani kuhusu jamii na mazingira yanayoizunguka. Waafrika wana ontolojia yao iliyokitwa katika dini na tamaduni zao (Kaponda, 2018). Dini imechanganua masuala yanayojibu maswali ya kiontolojia. Baadhi yake yanahusu nafasi ya Mwenyezi Mungu, roho, mizimu, binadamu, wanyama na vitu. Kiontolojia, Waafrika hawawezi kuishi bila ya dini kwa sababu binadamu hutambulika katika jamii kwa kushiriki katika imani, miviga, sherehe na matambiko. Dini ni mfumo wa itikadi, ushirikisho na matendo.

Jamii za Kimagharibi zilitumia ontolojia ya Kiafrika kumtazama Mwafrika kama nusu mtu. Suala hili lilisababishwa na kutokuwapo kwa taarifa muhimu kuhusu ontolojia ya Mwafrika (Sengo, 1995). Kila jamii ina ontolojia iwe imeandikwa au haikuandikwa. Hakuna ulazima wa kuitazama falsafa ya Kiafrika katika maandishi pekee. Jambo hili linatokana na ukweli kwamba miongoni mwa sifa za ontolojia ya Kiafrika ni dhana ya familia pana, kuthamini uzazi, imani kuhusu Mungu na mizimu ambayo huambatana na imani katika sihiri, uganga na tiba. Pia, kuna dhana ya wakati

na ujamiishaji wa kiduara. Kupitia sifa hizi, kila jamii ya Kiafrika inaweza kujipambanua kiontolojia. Makala hii imechunguza nafasi ya ontolojia ya Kiafrika kwa kurejelea jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania.

Mbinu na Nadharia ya Utafiti

Makala hii imechunguza kipengele cha ontolojia ya Kiafrika kwa kurejelea jamii ya Wanyakyusa nchini Tanzania. Mbinu za mahojiano na usaili zilitumika kupata data za msingi katika wilaya ya Rungwe na halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata sampuli ya watafiti waliotuwzesha kupata data kulingana na lengo mahsusi la makala. Nadharia ya Falsafa ya Kiafrika ilitumika katika uchambuzi na mjadala zilizowasilishwa. Mwasisi wa nadharia hiyo ni Placide Tempels mwaka 1945 (Lyamuya, 2021). Msingi mkuu wa nadharia hii kuchunguza namna falsafa ya Kiafrika inavyofungamana na kujibainisha vema katika mitindo ya maisha, misingi ya utamaduni, mifumo ya kisasa na kiuchumi, imani na mitazamo ya jamii kuhusu masuala ya kihistoria na kijiografia ya jamii inayohusika. Katika makala hii, nadharia hii imemuongoza mtafiti kuchunguza namna ontolojia ya Kiafrika inavyoakisi katika mitindo ya maisha, utamaduni na mazingira kwa kurejelea jamii ya Wanyakyusa.

Uwasilishaji wa Data

Makala hii imechunguza ontolojia kama dhana iliyotumika kuelezea masuala ya kijadi yaliyojengwa katika mfumo, mitindo ya maisha na utamaduni wa jamii ya Wanyakyusa. Uchunguzi umefanywa kubainisha mwelekeo maalumu wa kifalsafa kwa kurejelea mawazo na mielekeo ya fikra kwa kurejelea muktadha wa jamii teule. Mfumo na mitindo ya maisha inatazamwa kama kiini cha utambuzi wa mambo yanayounda na kubainisha falsafa ya jamii moja na nyingine, kijiografia na kihistoria. Mfano wa dhana hizo ni nguvu na siri ya uumbaji, nguvu ya maisha na uhusiano baina ya binadamu na mizimu. Nafasi ya ontolojia ya Kiafrika imeelezwa katika sehemu inayofuata.

Uumbaji na Nguvu ya Siri

Wanyakyusa wanaamini kuwa kuna nguvu za siri ndani ya uumbaji wowote. Jambo hili huitwa siri kwa sababu halieleweki kwa maarifa yanayopatikana kwa kutumia milango ya fahamu ya kupokea maarifa na taarifa (Oluwale, 1999). Nguvu inayopenya uumbaji wote ipo chini ya mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Mizimu na baadhi ya watu wamepeva kujua jinsi ya kuchota nguvu hiyo ili waweze kuitumia. Kwa kawaida, nguvu hii inakuja kwa njia ya vitu, mizimu au watu wenye uwezo wa pekee, wakiwamo wahubiri, waganga wa jadi na wachawi. Suala hili linagusa maisha baada ya kifo kwa kuwa roho za waliokufa zinaweza kutenda lolote kwa walio hai. Mizimu wana uwezo wa kugusa maisha ya walio hai kwa kuwa watu fulani wana vipawa vinavyowezesha kutumia nguvu fulani kubadilisha maisha ya binadamu wenzao.

Pia, wapo watu wenye uwezo wa kujua jinsi ya kutumia nguvu ya siri ili kutekeleza wanayotaka yafanyike. Matendo wanayofanya ni yale yasiyo ya kawaida ambayo

hayaeleweki kwa maarifa ya kisayansi wala hayatawaliwi na maarifa ya kawaida. Watu wenye vipawa hivyo hutumia namna za ibada kuleta nguvu hiyo ya pekee. Nguvu hizi hawakuumbwa nazo ila zinafunguliwa kwa njia ya kufanya kazi. Baadhi ya watu wenye uwezo wa kujua kutumia nguvu ya siri, hutumia vibaya kwa kusababisha matukio yenye kuleta mikosi, maradhi, vifo na ugomvi (Mair, 1969). Mara kwa mara, jamii inajaribu kuwaonya ili wasipite kiasi katika kufanya maovu. Uchawi unaosababisha maovu unastawisha hofu katika jamii. Waganga wana uwezo wa kuchota nguvu za siri ili kuleta mema na kudhibiti uharibifu unaoweza kusababishwa na wachawi.

Nguvu ya Maisha: Moyo, Nafsi na Ndoto

Kulingana na imani za jamii za Wanyakyusa, moyo huonesha nguvu ya rohani na ni asili ya matendo ya mwili na yote ya nafsi. Moyo unatengeneza hekima, busara, tamaa, chuki, hofu, ubaya na visasi (Mwambusye, 2013). Moyo ni mvuto unaoongoza mawazo ya mwanadamu hata matendo yake. Ndoto na nguvu ya maisha hutoka moyoni. Moyo unatengeneza nguvu ya maisha. Mambo mazito ya kiroho yakitokea yanaweza kutetemeshwa na hata kuuha moyo. Nafsi ni nguvu ya roho ambayo huuwezesha mwili kuishi. Moyo, nafsi na mwili ni kiumbe chenye uhai. Mtu akiugua sana tumaini huwapo ikiwa moyo na nafsi bado ipo. Hali ya moyo na nafsi ikianza kupungua na kutoweka, mtu anakufa.

Nafsi ni mchanganyiko wa kimwili na kiroho; na huondoka katika mwili wa binadamu akifa. Mtu akifa, maana yake, nafsi imeondoka. Kwa muda wa siku mbili, tatu au nne hivi, nafsi huzunguka pale pale penye msiba nyumbani pake au kwao mpaka afukuzwe kwa tambiko ili aende kuzimu (Mwabukusi, 2014). Sherehe hiyo ikikosekana, nafsi itaendelea kuzunguka na kuwatisha watoto na wanawake mpaka sherehe ya upatanisho itakapotolewa. Kwa upande mwingine, hiari yao, wachawi wana uwezo wa kuitenga nafsi yao na mwili. Hivi anaweza akawa amelala nyumbani wakati nafsi yake inawatembelea wengine, ikitenda itakavyo. Pia, nafsi za watu wa kawaida zinaweza kuondoka, hasa wakiota ndoto na kuona mambo ya ajabu katika safari zao.

Kuna maisha halisi ya mtu akiwa macho na akiwa usingizini. Ndoto si mawazo tu, bali ni matokeo ya maisha ya nafsi. Ndoto zinaweza kusababishwa na mawazo ya mtu akiwa macho. Mathalani, unaweza kuzungumza kuhusu mtu fulani na usiku anajitokeza katika ndoto. Watu waliokufa ambao wana shida nawe, wanaweza kukutokea katika ndoto ukiwa umelala. Mtu akisumbuliwa na ndoto, humwendea muaguzi ili afahamu asili na nia ya ndoto. Ndoto inaweza kukuelekeza, kukujulisha, kukudokeza, kukuonya na kukukataza jambo fulani (Abraham, 1994). Wapo watu wachache, wakiwemo watabiri, waganga na wanaoshikwa na pepo wenye ndoto zinazohusu mambo ya mbele.

Nguvu ya Sala, Sadaka na Tambiko

Sala na sadaka ni njia za kushirikiana na Mungu, mizimu na pepo (Mbiti, 1975). Sala zinazoelekezwa kwa Mwenyezi Mungu haziambatani na sadaka ila kwa mizimu. Sala

inaeleza sababu na nia ya sadaka. Sala na sadaka kwa pepo, asili zao zimeendelea kusahauliwa kwa kuwa taratibu zake hazieleweki ama zimeendelea kufifia sasa (Omoreghe, 1998). Madhumuni ya sala na sadaka yanatokana na kuharibika kwa taratibu za kawaida za maisha kama vile kupata mavuno haba, kuleta tumaini la mavuno mazuri, kutostawi kwa mifugo, vifo, utasa na ugumba. Pia, hushughulikia magonjwa na matatizo ya kujifungua au jamaa wakihangaika kwa ajili ya ndugu ambaye yuko mbali kwa shughuli fulani. Mtu akifuata ushauri kuhusu sala, sadaka, tambiko na dawa anaweza kuona matokeo mazuri kwa wakati muafaka.

Sadaka za kweli, wanyama wanachinjwa pale pale, ilhali za kusingizia, wanyama wanawekwa wakf. Kwa mizimu, sadaka zote mbili ni sawa kwa sababu wanyama waliowekwa wakf hutendwa tofauti na wengine. Kumweka mnyama wakf badala ya kumchinja ni faida ya wote. Mtu asiyemchinja mnyama wa pekee aliyewekwa wakf kama vile ng'ombe, mbuzi au kondoo anaweza kuzaa. Wakiwa wengi wanasaidia kupata wake wengi. Hivyo, watoto watakuwa wengi. Mizimu watakuwa na uhakika kwamba watashughulikiwa na kuheshimiwa kwa muda mrefu na vizazi vilivyopo na vijavyo. Ng'ombe au mnyama aliyewekwa wakf, hawezi kuuzwa wala kutolewa mahari. Wakimchinja au kumuuzwa kwa sababu yoyote, mizimu huarifiwa na kujulishwa mbadala wake.

Tambiko linahusishwa na kifo cha mnyama. Sadaka inahusisha vyakula pamoja na vitu vingine vinavyotolewa ambavyo si lazima uhai utolewe. Tambiko linategemea uzito wa tukio ama mwiko uliovunjwa kuhusu uhusiano baina ya Mungu, mizimu na roho kama umeharibiwa (Mwakanjuki, 2011). Wanyakyusa huamini kuwa chukizo lolote haliachwi bila kurekebishwa. Inajulikana wazi kuwa wizi, uchawi na kutokufuata miiko ya jamii ni kosa kwa Mungu na mizimu. Chukizo hilo lazima liondolewe kwa kutambika kwa Mungu au mizimu. Matukio kama ya kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu na kuwapo kwa magonjwa ya kuambukiza hujulikana kuwa ni pigo kutoka kwa Mungu. Tambiko hupaswa kufanywa kwa kuelekezwa kwa Mungu. Tambiko huongozwa na chifu baada ya kufanyika kwa mkutano kabla jua halijachomoza. Mkutano wa namna hiyo unalenga kubaini sababu za kutokea kwa hali au matukio yaliyopo kabla ya kufanya tambiko.

Mara kwa mara, hawezi kujua kitu kinachotakiwa kutolewa kulingana na kosa lililofanyika. Wapiga bao na watambuzi ndiyo wanaohusika kusema kitu cha kutoa kwa tambiko au sadaka. Misingi ya kufanya tambiko kwa Wanyakyusa hutegemea mambo kadha. Kwanza, hulenga kuziba mpasuko uliopo kati ya Mungu na watu, watu na mizimu ambao husababishwa na makosa yaliyokwishafanyika. Makosa hayo husababisha kuvunjika kwa uhusiano na ushirikiano baina ya Mungu, binadamu na mizimu. Pili, hutambika ili kutaka ushirikiano kati ya Mungu na watu au kati ya watu na mizimu. Tatu, kutambika ni njia mojawapo ya kumshukuru Mungu au mizimu kwa ajili ya mema fulani ambayo mtambikaji ameona kuwa ametendewa. Mara nyingi sadaka na matambiko yanatolewa kwa Mungu kwa ajili ya upatanisho, shukrani na kushirikiana na Mungu. Sadaka zinahesabiwa kuwa ni zawadi kwa Mungu kwa sababu kila jambo na mafaniko yote hutokana naye.

Chimbuko la Mnyakyusa wa Kwanza

Kuna nadharia kuu mbili kuhusu chimbuko la Mnyakyusa wa kwanza (Meyer, 1993). Nadharia ya kwanza inadai kwamba Mungu aliumba ulimwengu wote. Binadamu wa kwanza alitoka sehemu za ziwa Nyasa. Pale, ziwa Nyasa, ndipo walipoishi watu wa kwanza, Lyambilo na mkewe Ngogotike. Binadamu hao waliishi pamoja na wanyama kwa amani. Simba na wanyama wengine wala nyama walikuwa wanakula majani tu. Mungu aliwapatia binadamu kila kitu. Mahali walipoishi panaitwa mawe ya Mungu. Mwanzoni watu wa kwanza walikuwa hawafi, ila walipoanza kula nyama na kuwinda wanyama. Hali ya kiparadiso iliisha na uadui uliingia kati ya mwanadamu na wanyama.

Nadharia ya pili inaeleza kuwa dunia ilipoanza kuwako, Mungu aliishi juu ya mlima Rungwe. Mungu alipiga nyuzi za mgomba kwa kijiti akiketi katika mlima Rungwe. Alipokuwa akipiga, mara walitokea wanaume wawili kwenye nyasi za mlima huo. Siku ilipoendelea, Mungu akapiga tena, akatokea mwanamke mjamzito ambaye baadaye alimzaa mtoto wa kike. Mwanaume mmoja kati ya wale wawili alimwoa yule mwanamke na wa pili alimwoa mtoto wa yule mwanamke alipokuwa amekua. Waliteremka mpaka Fiti karibu na kreta ndogo ya mlima Rungwe. Toka huko waliteremka tena mpaka Kabale chanzo cha mto Suma mahali ambapo siku hizi pana kijiji cha Banyakajila au Banyakyolo. Kutoka huko, waliendelea kuzaliana zaidi na zaidi katika Unyakyusa yote ya leo.

Asili ya kutoka Rungwe inathibitishwa hata katika mapokeo mengine. Watu wanasema mimi kutoka Rungwe, nimesema mimi niliyeteremka kutoka Rungwe au nimesema, mimi kutoka Kabale. Zaidi ya hayo, ni desturi ya Wanyakyusa wengi kuchimba kaburi kwa jinsi ya kuhakikisha kwamba kichwa cha maiti kinaelekezwa mlima Rungwe. Hata kwa Wanyakyusa wa ziwani (Kyela), mlima Rungwe una maana maalumu kwa mazishi. Hata wao wanalaza maiti kuelekea mlima Rungwe. Wakiulizwa, wanasema ndiko tulikutoka.

Baada Kifo: Mfu-hai

Binadamu akiwa hai huishi duniani, ndivyo waliofariki hukaa huko kuzimu. Maisha ya kuzimu ni sawa na maisha ya hapa duniani, isipokuwa mizimu hawana mwili. Maisha ya hapa duniani yanamalizika na mauti. Hali ya maisha ya kuzimu hutegemea sana hali ya maisha ilivyokuwa duniani (Mwakasaka, 1999). Kama ilikuwa nzuri hapa duniani, hata huko itakuwa nzuri. Kifo kinapomchukua mtu, mtu yule huwa mfu-hai (Mbiti, 1970). Wafu kuweza kuongea na walio hai kawa njia mbalimbali. Walio hai huongea na wafu kwa njia ya maombi na sadaka. Hali hii inatokana na kuwa yeye ni roho kwa sababu haonekani, ingawa huendelea kuwa na hali ambazo humfanya ajulikane kimwili.

Kuna utengano mkubwa kati ya wafu na walio hai. Mfu-hai anaweza kutokea kwa watu wa nyumbani kwake. Tukio hilo si la furaha kwa watu hai. Roho za wafu hazisalimiwi wala mtu hai kutuma salamu zake kwa roho za wafu. Kuna uhusiano mkubwa baina ya wafu-hai na walio hai. Wafu-hai huwa kiungo kati ya binadamu

walio hai na Mungu. Walio hai huonesha ushirikiano wao na wafu-hai kwa njia ya sadaka, matambiko na sala. Hali ya kuwapo mfu-hai huendelea kuwapo miongoni mwa walio hai mpaka afe mtu wa mwisho aliyewakumbuka (Bodunrin, 1981). Baada ya hapo, wafu-hai huanza kuzama ndani ya wakati wa zamani kwa kuwa hakuna atakayemkumbuka. Katika hatua hii, anakuwa roho katika ulimwengu wa roho kamili. Hakuna zaidi ya ngazi ya kuwa roho. Ngazi iliyo mbele ya roho ni Mungu. Katika mawazo ya Kiafrika hakuna tarajio wala uwezekano wa mtu kushiriki katika uungu wa Mungu. Mungu ni juu ya hali zote za maisha.

Mtoto akizaliwa hupokelewa katika jamaa kwa vitendo na ishara mbalimbali za kijadi. Anapopata kuwa mtu mzima anaweza kuoia ili kuendeleza na kuongeza jamaa. Ndoa inamuunganisha na wale waliokwishafariki na watakozaliwa naye. Jambo linalotazamiwa baada ya hapo ni kifo. Kifo husimama kati ya walio hai na roho za watu waliofariki. Kifo ni ngazi kati ya maisha ya kimwili na ya wafu-hai. Mtu akikaribia kufa, jamaa yake hukaa karibu na kitanda chake. Huwapo hapo kuchunguza kisa cha ugonjwa ili kuchukua hatua za kuuzuia, ikiwa kitatokana na uchawi. Kuwapo kwa mtoto wake wa kwanza karibu naye ni ishara kuwa ikiwa atakufa atakuwa anaishi kwa njia ya watoto wake.

Kulingana na imani za Kiafrika, kifo cha kawaida ni cha uzeeni. Vifo vingine ni matokeo ya uchawi, mizimu au adui yeyote. Kifo kikitokea mganga hualikwa kutoa mashauri yake ili yaliyosababisha kifo yaepukwe (Mwangosi, 2019). Kifo kikitokea kilio huanza. Makusudi ya kilio katika jamii nyingi ni mengi. Kwanza, huonesha huzuni. Pili, huonesha kuwa hawahusiki na sababu za kifo hicho. Tatu, ni njia ya kuwakaribisha watu katika msiba. Nne, kumbembeleza aliyekufa ndio maana waombolezaji huambatanisha kilio chao na maneno maalumu kuhusu aliyefariki. Mila na desturi za kuzika hutofautiana miongoni mwa jamii za Kiafrika. Kifo hakileti mwisho wa kuishi bali ni badiliko tu la maisha. Baada ya kuendelea kuishi kimwili, kifo kinamwingiza mtu katika hali nyingine ya maisha. Kuna hatua ya kuishi mfu-hai na baadaye kuishi kiroho.

Kifo si cha kutisha kwa Mwafrika. Mapokeo ya baadhi ya Wanyakyusa husema kuwa wabaya na wema wana nafasi ya kuendelea kuishi kama wafu-hai na baadaye kama roho. Tofauti iliyopo ni kwamba wema huishi maisha yasiyo ya dhiki. Waovu hutaabika hata katika maisha hayo ya kiroho. Pia, wanaamini kuwa wafu-hai wanaishi karibu na Mungu kuliko waliohai. Hali hiyo huwafanya walio hai kuomba kushirikiana na Mungu kupitia wafu-hai. Mapokeo ya Wakristo wa kanisa la Roma kumuomba Mungu kupitia kwa Watakatifu ni jambo lisilokwaza imani za jamii za Kiafrika.

Uchawi, Uganga na Tiba

Wanyakyusa daima huogopa sana uchawi kuliko wanavyoogopa matendo ya Mungu na usumbufu wa mizimu. Mtu anahatarishwa kwa uchawi tangu kuzaliwa hata kufa. Kutokana na uchawi, hakuna penye usalama wala kazi iliyo salama. Kila sehemu ya maisha imehatarishwa kutokana na uchawi (Peterson, 1992). Kila mtu anapaswa

kujihami na kujikinga kwa dawa yenye uwezo wa kuzuia uchawi. Dawa za kuondoa uchawi ni nyingi kama zilivyo dawa za kulogea. Wasaidizi wa kwanza wa mtu wa kawaida ni waganga. Kazi yao ni kujua nguvu ya dawa, yaani joka lililo ndani ya binadamu, wanyama, mimea na ya vitu visivyo hai. Kazi ya waganga ni kuzifahamu nguvu hizo, kuziweka huru, kuziunganisha na kuziongoza ili zifanye kazi. Ustadi huo unamfanya mganga aheshimiwe na kuogopwa.

Licha ya waganga kukubaliwa, wapo wanaofanya kazi yao sirini kwa kujivuna na kwa kupenda kuharibu. Hao wanaitwa walozi, nao huogopwa sana kwa sababu matendo yao yamefichika na inashindikana kuwazuia. Mlozi akigunduliwa na kuadhibiwa watu hufurahi sana. Uganga unarithishwa, ingawa wengine wanaweza kujifunza kwa malipo. Waganga na wachawi wanaeleza kuwa wanapata maarifa na ujuzi huo kutoka kwa Mwenyezi Mungu (Oyekwe, 1975). Waganga wabaya wanaweza kutumia dawa kali na wana uwezo hata kuwaua watu, ingawa wengine hawau licha ya kuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Pia, wapo waumbaji wa wanyama, watengenezaji wa mvua na wanaopasua maiti ili kubaini sababu za ugonjwa na kifo. Majukumu yao mengine ni kudhibiti wezi wa mazao, mifugo, kutatua ugomvi, kumrudisha mke akitoroka na kuzindika nyumba.

Shughuli za uganga huambatana sana na ibada za jadi za kusalia miungu kiasi cha kuwa sehemu mojawapo muhimu. Kuna aina sita za waganga wanaogawanyika katika makundi mawili (Nkwera, 2002). Kundi la kwanza ni la waganga wanaoponya magonjwa. Hao ndio waganga wa mitishamba, waombezi, madaktari na wauguzi. Waombezi ni watu waliokirimiwa uwezo na Mwenyezi Mungu wa kuponya magonjwa na udhaifu mbalimbali kwa njia ya sala, kufunga na kujinyima mambo mengi ya kidunia. Waombezi wanaweza kulinganishwa na wahubiri mashuhuri katika makanisa ya Kikristo. Kundi hili halina ushirika na kuisalia miungu, mizimu ama mapepo. Hawa hawajitukuzi wala kubabaisha wateja. Wao huzingatia kiini cha utabibu.

Kundi la pili ni la wale wanaojishughulisha sana na majini na mizimu. Kwa bahati mbaya, mizimu wenyewe aghalabu ni shetani anayejifanya mzimu. Hujiita pia kwa kuficha undani wao kupitia waganga wa kitamaduni, wajuzi wa mazingara au wataalamu wa kienyeji. Katika kundi hili la pili, wamo pia wapiga ramli, walozi na wachawi. Kundi hili lina ushirika mkubwa na ibada za kusalia miungu na kuwaita wahenga. Mungu mwenye kusaliwa hapa ni jini, si Mwenyezi Mungu. Shabaha ya kutenda na mazoea yao ni kumtukuza awali ya yote jini, kuseta mioyo ya wateja wao ili wawatii, kupotosha imani na kuchuma fedha na mali. Udanganyifu na utapeli vina nafasi kubwa katika kundi hili.

Kulingana na imani za Waafrika magonjwa yana sababu za kiroho. Ugonjwa unatokana na kusudi la mtu au mizimu kulipiza kisasi kwa sababu ya uhusiano mbaya (Asante, 1993). Wajibu wa mganga ni kutambua namna ya ugonjwa na sababu zake. Pia, kutambua uhusiano mbaya katika mazingira ya mgonjwa unaoleta matatizo. Akiisha tambua sababu za ugonjwa, atumie utaalumu wake katika kuponya na

kutumia uwezo wake kumudu harakati za kuwalinda watu kutokana na wachawi na mizimu wanaolenga kumwingilia mtu na kumtawala. Wachawi hawahesabiki kama waganga. Hutazama kama waharibifu kwa sababu wanajisifu kwa matendo yao yanayoleta madhara kwa jamii. Sehemu kubwa ya kazi yao wanaifanya usiku, ingawa hata mchana wanaweza kuharibu kwa mtupo mbaya wa jicho. Ubaya wa kazi walozi unaonekana wazi katika lugha. Tamko la kumchukiza mtu sana ni kumwambia kuwa wewe ni mchawi. Kuna hirizi za kujikinga ambazo zinawaliwa shingoni au kuangikwa nyumbani. Mtu wa kawaida anaweza kuota ndoto inayomfumua kutambua kuwa fulani ni mchawi.

Kuzimu na Mizimu

Mahali pa mizimu ni kuzimu, ulimwengu wa chini. Watu wote lazima waingie pale, ingawa hapapendwi. Pia, huitwa nchi ya asili kwa sababu kila mtu atakwenda huko. Inaonekana Mungu aliwapa mizimu Kuzimu kama mahali pao kama alivyowapa walio hai dunia. Kuzimu hakufahamiki, isipokuwa inaeleweka wazi kwamba njia ya kufika pale inakwenda chini. Kifo huweka mipaka kati ya walio hai na wafu. Kufa ni utengano mzito sana, ila ni kimwili na kimahali tu (Masolo, 1994). Mtazamo huu unatoka na kwamba aliyefariki huendelea kushirikiana na walio hai kwa njia ya ndoto. Kaburi lenyewe ni mahali pa muda tu kwa roho ya marehemu kabla haijaingia kuzimu. Kulingana na mila za kuzika za Wanyakusa zinaonesha kuwa mwingilio wa kufika Kuzimu ni mlima Rungwe. Kaburi lenyewe hutengeneza nafasi maalum, ambapo kichwa lazima ikelekezwe katika mlima Rungwe. Kuzimu, mzimu hupokelewa na ndugu zake waliotangulia. Ili apokelewe vizuri, walio hai huomba katika maombolezo yao. Wapo hata wanaodai kuwa wamefika kuzimu na kurudi. Mwanamke alikufa pamoja na mtoto wake kutokana na ugonjwa wa ndui alieleza hivi:

Kuzimu si mbali, ni karibu sana. Nilifika kule na mtoto wangu kwenye mti wa kijiji. Kule tulisubiri. Akaja kijana aliyeniambia, ngoja nikakuchukulie maziwa. Nilisubiri kwa masaa kadhaa, nisipate maziwa. Baadaye, likaja kundi la watoto kutoka kijijini kwa furaha. Walipomwona mtoto wangu walimchukua, wakaenda naye kijijini kwa furaha. Kwangu walikuja baadaye (aliwataja majina baadhi ya watu waliofariki kabla yake), wakaniuliza, unataka nini hapa? Angetangulia kufika mume wako. Kwa hiyo, ilibidi nirudi duniani, nikaamka tena. Tayari, maombolezo ya mtoto wangu aliyechukuliwa na kundi la wenzake yalikuwa yakiendelea (Meyer, 1993: 66).

Wengine wanaeleza hivi:

Ukifika kuzimu, kwanza unakutana na wageni wanaokuuliza, wako wapi rafiki zako ili wakupokee? Wakija rafiki zako na kukutambua, wakiita kwa furaha, wa kwetu! Wa kwetu! Basi utaenda nao kijijini. Wasipokupokea, wasipokukaribisha chakula, wakikupa kisogo, unapaswa kuamka tena na kuendelea na maisha ya walio hai (Meyer, 1993: 67).

Nchi ya kuzimu inafanana na nchi ya walio hai. Maongezi ya kawaida yanafuata mfumo ule ule kama mahali pengine duniani. Tofauti moja kubwa ni kwamba vitu vyote, miti, nyumba, migomba, wanyama na binadamu ni vivuli. Kuzimu kunadumu milele, isipokuwa wakazi wake. Baada ya muda fulani, mizimu waliokaa sana wanabadilika na kuwa kama wadudu. Uhusiano baina ya walio hai na mizimu kiini chake ni ulinganifu mkubwa uliopo katika jamii ambao haupunguzwi kwa kifo (Mwambusye, 2006). Baba, mama na watoto wanaendelea kuwa na umoja hata kama wengine wako duniani au kuzimuni. Mizimu wako huru kufika duniani usiku na kujishughulisha kwa faida au hasara ya walio hai. Mizimu wanaweza kusaidia katika mambo mengi. Wanaweza kuchukua na kuleta uharibifu mwingi kama hawathaminiwi. Uzembe, uhalifu na maneno mabaya dhidi ya mizimu na ugomvi katika jamaa huadhibiwa na mizimu. Pia, wanaweza kutia moyo, kuonya na kudokeza tukio au jambo kwa njia mbalimbali. Mathalani, nyoka aliyekinga njia ni ishara ya kukataza jambo linalipaswa kufanywa. Mizimu wanaweza kuonekana hadharani. Kwa mfano:

Isela alitaka ndizi kwa rafiki yake Mapepo. Alikutana naye njiani. Walisalimiana na kuzungumza masuala kadha. Kisha, Mapepo alimwambia atapata ndizi kwake. Wakaagana. Kufika kijijini, kulikuwa na msiba. Aliuliza aliyefariki. Aliambiwa kuwa Mapepo amefariki. Alishtuka mno! Akasema, mbona nimekutana naye njiani! Kufika nyumbani kwake aliugua sana kwa sababu badala ya kunyamaza kuhusu tukio hilo, alizungumza. Alipaswa kunyamaza na kutohudhuria msiba (Meyer, 1993: 69).

Mizimu wana hali ya juu kuliko walio hai kwa kuwa idadi yao ni kubwa kuliko walio hai duniani. Pia, wana ujuzi na hekima ya hali ya juu kwa sababu vizazi vingi vinachangia. Mizimu wana uhuru mkubwa kuzunguka zunguka kwa sababu hawakufungwa tena katika mwili. Hali hiyo, huwafanya walio hai kuwanyenyekea, kujali mapenzi yao na kutii mizimu. Hata katika mazishi, pamoja na watu kuonesha uchungu kwa ajili ya ndugu yao kuondoka na hofu juu ya kifo, pia wanahofu ya marehemu aliyegeuka mzimu. Kiongozi wa taratibu zote kuhusiana na mizimu kwa kawaida ni mzee wa ukoo. Huarifiwa matatizo yote ili apeleke mbele ya mizimu. Mwanamke anaweza kuomba mizimu wa ukoo wa mume wake. Katika kufanya hivi, wanatangulia kusema, 'Nimeazima moto kwako', yaani nakuletea tatizo kutoka katika nyumba yako.

Hitimisho

Makala hii imechunguza mitazamo mbalimbali kuhusu maisha, utamaduni na falsafa katika jamii ya Wanyakyusa. Mambo hayo ni ya msingi katika kuijenga na kuiendeleza jamii kimaadili, kiutamaduni na kimaisha ili kuyakabili maisha na mazingira yao. Uchunguzi uliofanywa unaonesha kuwa ontolojia ya Kiafrika katika jamii iliyolengwa hutazamwa kama chombo thabiti cha urejelezi wa masuala ya kiasili na kiutamaduni yanayotumika kama kiungo cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuimarisha na kuiweka jamii pamoja kimaisha na kiutamaduni. Baadhi ya masuala yaliyochunguzwa yanahusu kuzimu na mizimu, uchawi, uganga na tiba, maisha baada kifo, nguvu ya sala, sadaka na tambiko. Masuala haya yanatendeka kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya kila siku ya jamii.

Marejeleo

- Abraham, R.G. (1994). *Witchcraft in Contemporary Tanzania*. Cambridge: African Studies Centre.
- Asante, K. W. (1993). *The African Aesthetic: Keeper of the Traditions*. ABC – CLIO: Incorporate.
- Bodunrin, P. (1981). The Question of African Philosophy. Katika *The Essential Reading*. New York: Paragon Publishers uk. 213.
- Faustine, S. (2017). Usawiri wa Falsafa ya Kiafrika na Mchango wake katika Riwaya ya Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Hountondji, P. (1983). *African Philosophy, Myth and Reality*. London: Hutchison University Library for Africa.
- Kaponda, G. (2018). Ontolojia ya Kiafrika katika Mbolezi za Wanyasa. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Lyamuya, H. N. (2021). Dhima ya Falsafa ya Kiafrika katika Jamii: Mifano Kutoka katika Tendi za Kiswahili. RUJASS, Vol 7: Issue 1, 135 – 147.
- Magesa, L. (1997). *African Religion the Moral Traditions of Abundant Life*. New York: Orbis Books.
- Mair, L. (1969). *Witchcraft*. London: World University Library.
- Makumba, M. M. (2005). *Introduction to Philosophy*. Nairobi: Paulines Publications.
- Masolo, D. A. (1994). *African Philosophy in Search of Identity*. Blomington and Indianapolis: Indiana University Press.
- Mbiti, J. (1970). *Introduction to African Religion*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Mbiti, J. (1975). *Introduction to African Religions*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Meyer, T. (1993). *Wa-Konde: Maisha, Mila na Desturi za Wanyakyusa*. Mbeya: Moravian Theological College.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Mwabukusi, A. (2014). Nyimbo za Kazi Katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji.
- Mwakanjuki, N. (2011). Athari za Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi kwa Nyimbo za Kapote za Mwimbaji Mwandwanga katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mwakasaka, C. S. (1977). *The Oral Literature of Banyakyusa*. A Research of Master Degree, University of Dar es Salaam.
- Mwambusye, D. (2006). *A Guide to Nyakyusa Cultural Heritage*. Tukuyu: Tukuyu Highland Press.

- Mwambusye, D. (2013). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kinyakyusa*. Tukuyu: Tukyu Highland Press.
- Mwangosi, G. (2019). Mwanamke, Uchumba, Uzazi na Malezi katika Misemo ya Jamii ya Wanyakyusa. *RUJASS*, Vol 2: 27 - 34.
- Nkwera, F. (2002). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: Busines Printers Limited.
- Oje-Ade, F. (2004). *Being Black Being Human: More Essays on Black Culture*. Trenton New Jersey: African World Press Inc.
- Oluwale, S. (1999). *The Africanness of A Philosophy*. Logos: Ark Publications.
- Omogbe, J. (1998). 'African Philosophy: Yesterday and Today' katika *AfricanPhilosophy: An Anthology*. Cambridge: Blackwell Publishers.Uk. 5 - 11.
- Oyekye, K. (1975). African Religious and Philosophy by J. S. Mbiti. Book Review katika *Second Order*, Vol. 4, No. 1.
- Peterson, D. (1992). *Theolojia ya Kikristo katika Mazingira ya Kiafrika*. Nairobi: Baptist House.
- Sengo, T. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. TUKI: Dar es Salaam.